# Dhima za Vibainishi Vioneshi katika Kiswahili Sanifu

*Adventina Y. Buberwa*[1] na *Shaibu I. Champunga*[2]
[1]*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*
[2]*Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam*

**Ikisiri**

**Makala haya yamenuia kuchunguza vibainishi vioneshi katika lugha ya Kiswahili ili kubaini dhima za vibainishi hivyo. Lengo hasa likiwa ni kujaribu kudhukuru dhima za vibainishi vioneshi ambapo mara nyingi wataalam huelezea dhima moja ya vibainishi ambayo ni kuonesha masafa ya ukaribu au umbali. Data za makala haya yalikusanywa maktabani kutoka katika matini za vitabu vya Kichwamaji (Kezilahabi, 1974) na Kivuli Kinaishi (Mohamed, 1990). Mbinu iliyotumika ni usomaji wa maandiko na kunukuu madondoo yanayohusiana na dhima za vibainishi vioneshi. Data hizo zilichambuliwa kwa mbinu ya maelezo. Nadharia ya Mofolojia Leksika iliyoasisiwa na Kiparsky (1982) ilitumika. Kwa muhtasari, matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kwamba vibainishi vioneshi vina dhima mbalimbali ikiwa ni pamoja na dhima ya kuonesha mahali, dhima ya kuhimiza, msisitizo, kuunganisha na kuonesha umbali au ukaribu wa kitu. Makala haya yanapendekeza kwamba, utafiti mwingine ufanyike katika aina zingine za vibainishi ili kupata maarifa majumui kuhusu dhima za vibainishi hivyo katika lugha ya Kiswahili. Pia, utafiti unaweza kufanywa kuchunguza dhima za vibainishi katika lugha mbalimbali za Kibantu ili kuona namna dhima zinavyoweza kutofautiana na/au kufanana na zile za lugha ya Kiswahili.**

**Maneno Muhimu:** Vibainishi, Vioneshi, Kiswahili, Mofolojia

**Utangulizi**

Kumekuwa na mitazamo inayohitilafiana baina ya wanaisimu kuhusu vibainishi vioneshi. Tukianza na fasili ya vibainishi vioneshi, mitazamo miwili inadhihirika, mtazamo wa kwanza unawakilishwa na wanaisimu kama vile Kraal (2005) na Khamis (2011). Hawa wanavichukulia vibainishi vioneshi kuwa ni maneno yenye sifa ya kuonesha kitu fulani cha karibu au mbali na eneo la mzungumzaji au msikilizaji. Wanatoa mfano wa maneno kama *huyu, huyo,* na *yule*. Fasili hii imeegemezwa zaidi katika kazi au dhima za maneno hayo kwa kuyatazama yakiwa pwekepweke.

Kwa upande mwingine, wanaisimu kama vile Thompson na Shchleicher (2001), Habwe na Karanja (2012) na Wesana-Chomi (2013) wanaona kwamba vibainishi vioneshi ni viwakilishi vioneshi au vivumishi vioneshi katika sentensi. Wanatoa mifano katika sentensi 'Watu *wale* ni wageni' na 'Viatu *hivi* vinanuka'. Maneno *wale* na *hivi* yametumika kama vivumishi katika sentensi. Bila shaka, fasili hii inatofautiana na fasili ya awali ambapo fasili imeelekezwa katika kuvitazama vibainishi vioneshi katika muktadha wa tungo mbalimbali. Fasili hii ya pili inaweka pamoja maneno *huyu, hiki, mle, mzuri, bora, mrefu* na kadhalika kuwa katika kategoria moja ya vivumishi au viwakilishi. Kwa hakika, mtazamo huu umekitwa katika mkabala wa kisintaksia wa kuainisha maneno kwa kuzingatia nafasi yake katika tungo, jambo ambalo linasababisha kuvichanganya vibainishi vioneshi katika kategoria ya viwakilishi na vivumishi. Kwa muktadha huo, makala haya yanaunga mkono mtazamo wa Kraal (2005) na Khamis (2011) kwa kuwa vibainishi vioneshi ni kategoria ya maneno inayojitegemea ambayo inaweza kubadilika kulingana na nafasi yake katika tungo kama zilivyo aina nyingine za maneno.

Kwa upande wa dhima za vibainishi vioneshi, wataalamu wengi wanaelekea kukubaliana kuwa kuna dhima moja tu ya kuonesha masafa. Mathalani Mgullu (1999), Massamba (2004), Thompson na Shchleicher (2001), Habwe na Karanja (2012) na Wesana-Chomi (2013) wanabainisha dhima ya masafa katika lugha ya Kiswahili wakionesha kuwa vibainishi vioneshi huonesha umbali na ukaribu baina ya mzungumzaji na msikilizaji. Tofauti hizi zinatokana na mikabala wanayoitumia wataalamu

wanaohusika. Hali hii imesababisha kutokea kwa ukinzani ambao ndio umechochea udadisi wa watafiti kushughulikia kipengele hiki madhukura.

Kwa hiyo, makala haya yanajaribu kuangazia vibainishi vioneshi vya Kiswahili kwa kutumia data za zilizokusanywa kwa njia ya kusoma na kuchambua matini. Mbinu hii ilitumika kwa sababu chanzo cha data ya utafiti huu ni matini zilizoandikwa zenye vibainishi vioneshi vya Kiswahili. Katika mbinu hii, vitabu vilivyopitiwa ni tamthiliya moja ya *Kivuli Kinaishi* na riwaya moja ya *Kichwamaji*. Katika vitabu hivyo, kila kibainishi kilichojitokeza kilibainishwa na kutambua dhima za kila kibainishi. Kupitia mbinu hii, vibainishi 54 kutoka vitabu vyote viwili vilibainishwa. Kati ya vibainishi 54, vibainishi 27 vilichukuliwa kutoka kila kitabu.Vibainishi vilivyoshughulikiwa viliteuliwa kinasibu kwa kuwa kila kibainishi kilikuwa na nafasi ya kuteuliwa.

Uchanganuzi wa data zilizokusanywa uliongozwa na nadharia ya Mofolojia Leksika (ML). ML ni nadharia ya mofolojia ambayo imetumiwa na Kiparsky (1982) katika kazi zake kuchambua data za lugha. Hii ni nadharia zalishi na nyambulishi inayohusisha kiwango cha mofolojia kama kiwango mahsusi cha lugha. Nadharia hii inaonesha kuwapo kwa uhusiano wa kanuni zinazojenga maumbo ya kimofolojia, na sheria hizo zinadhibiti maumbo hayo. (Katamba na Stonham, 2006). Kanuni zote hizi hutumika kuonesha mipaka yenye kusadifu sarufi ya lugha inayohusika. Nadharia hii inatoa mwanga na mwelekeo wa kufafanua muundo wa maneno katika lugha unaoleta maana. Muundo wa maneno unahusisha muungano wa mofimu katika ngazi ya neno, maana na kanuni za lugha inayohusika. Utafiti huu ulilenga kuchunguza upya dhima za vibainishi vioneshi vya Kiswahili. Kwa hiyo, nadharia hii imemuongoza mtafiti kubaini maumbo yanayounda vibainishi vioneshi yenye kuleta maana katika lugha ya Kiswahili, na dhima za vibainishi hivyo.

Mofolojia Leksika ni nadharia ambayo inamilikiwa na misingi kadhaa ya kanuni zinazounda maneno. Baadhi ya kanuni zimeainishwa na Buberwa (2014, 2016) kwa kutaja mihimili mitano ambayo ni mhimili wa ngazi leksika, mhimili wa mzunguko kamili, mhimili wa kufuta mabano, mhimili wa ufinyu wa sifa na mhimili wa kuhifadhi muundo. Hata hivyo, mhimili ambao umetumika katika utafiti huu ni mhimili wa mhimili wa kuhifadhi muundo.

Mhimili wa kuhifadhi muundo unahusika katika kuunda muundo sahihi unaokubalika katika lugha. Mhimili huu husisitiza taratibu za kuunda maneno yenye maana kamili. Hivyo basi, moja ya sifa zinazohusiana na muundo wa neno na kanuni zinazotawala mchakato wa uundaji wa maneno ni mhimili wa kuhifadhi muundo. Mhimili huu huonesha kuwa muunganiko wa sauti au mofimu sharti upangiliwe katika utaratibu unaukubalika na sarufi ya lugha husika katika kuunda maneno. Mhimili huu hauruhusu uundaji wa maneno yasiyokubalika katika sarufi ya lugha. Kinachokusudiwa hapa ni kwamba, maumbo au mofu zinazowakilisha mofimu za maneno lazima zipangwe katika mfuatano unaokubalika ili kuleta maaana katika sarufi ya lugha husika. Kwa mujibu wa makala hii, vibainishi vioneshi vya Kiswahili hujitokeza katika mpangilio kulingana na sarufi ya lugha husika. Kwa hiyo, mhimili huu umeongoza vyema uchanganuzi wa data na imebainika kwamba sauti na mpangilio wa mofimu katika vibainishi vioneshi vya lugha ya Kiswahili umezingatia muundo mwafaka wa sarufi ya Kiswahili.

**Dhana ya Vibainishi**

Dhana ya vibainishi ilianza kutumika katika karne ya 20, hasa baada ya kuibuka kwa Sarufi Geuzi Zalishi iliyoasisiwa na Chomsky (1965). Wanasarufi Geuzi Zalishi waliona kuwa kulikuwa na haja ya kuwa na dhana ya kibainishi kama aina mojawapo ya maneno iliyotofauti na dhana ya kivumishi (Philipo, 2015). Kwa hiyo, dhana hii ya vibainishi kama kategoria inayojitegemea ni mpya katika isimu, hususan katika lugha ya Kiswahili kwani imeshughulikiwa na wataalamu wachache kama vile Khamis (2011) na Philipo (2015). Hii ni kutokana na sababu kwamba wanaisimu wengi wamechanganya dhana hii ya vibainishi na vivumishi pamoja na viwakilishi. Wanaisimu mbalimbali wamefasili dhana ya vibainishi katika lugha mbalimbali ulimwenguni. Mathalani, Richards na Schmidt (2002) wanafasili kibainishi kuwa ni neno ambalo hutumika pamoja na nomino na ambalo kwa kiasi fulani huonesha ukomo wa maana ya nomino. Khamis (keshatajwa) anafasili vibainishi

kuwa ni neno lenye kufanya kazi ya kutambulisha jina au kiwakilishi au kielezi au kibainishi kingine kwenye tungo. Kutokana na fasili hizi mbili, tunaweza kupata fasili ya jumla ya vibainishi kuwa ni aina ya maneno yanayofanya kazi ya kufafanua kitu kiidadi au kutambulisha nomino. Kwa mfano:

1 (a) Mtoto **huyu** ni mkorofi.
(b) Wanafunzi **hawa** ni werevu.
(c) Askari **wote** ni viwavi.
(d) Duka **lipi** lina punguzo la bei?

Katika mfano wa 1, maneno yaliyokozwa wino ni vibainishi katika lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, makala haya yamechunguza vibainishi kama kategoria ya maneno inayojitegemea na ina aina zake zenye dhima mbalimbali.

Wataalamu wengi (taz. Timoth, 1987; Richards na Schmidt, 2002; Khamis, 2011; Philipo, 2015; Strom, 2015; Mwamzandi, 2018) wameainisha vibainishi katika lugha mbalimbali ulimwenguni, Kiswahili kikiwemo. Ingawa wametofautiana kiidadi na kwa matumizi ya istilahi za vibainishi hivyo, wanakaribia kufanana katika uanishaji wao kiuamilifu. Kwa mfano, Richards na Schmidt (2002) wanaainisha aina kuu tano za vibainishi katika lugha ya Kiingereza ambazo ni:

2 (i) Vibainisho[1]
(ii) Vibainishi vioneshi, mfano: hili, ule
(iii) Vibainishi vimilikishi, mfano: yake, yao n.k
(iv) Vibainishi kiasi, mfano: nyingi, yoyote, mengine.
(v) Vibainishi vya numerali, mfano: mmoja, watatu, n.k.

**Chanzo:** Richards na Schmidt (2002:152) (Tafsiri yetu)

Katika mfano wa (2) hapo juu tunaona kuna aina tano za vibainishi. Aina (i) tumeshindwa kuonesha mfano wake kwa kuwa aina hii ya vibainishi haipo katika lugha ya Kiswahili. Aina hii inapatikana katika lugha ya Kiingereza ambayo hata Massamba (2004) anataja kwamba *a*, *an* na *the* ni vibainishi katika lugha ya Kiingereza, ambavyo havina maana ya kileksika vikisimama peke yake. Hivyo basi, vibainishi hivyo lazima viandamane na nomino ndipo viweze kuleta maana kamili. Makala haya yalijihusisha na uchunguzi wa dhima za vibainishi vioneshi katika lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, aina zingine za vibainishi hazikushughulikiwa. Sehemu inayofuata inaangazia dhana ya vibainishi vioneshi.

**Dhana ya Vibainishi Vioneshi**

Vibainishi vioneshi katika lugha za Kibantu na zisizo za Kibantu vimejadiliwa na baadhi ya wataalamu. Mathalani, Kraal (2005) alifanya utafiti katika lugha ya Kimakonde kuhusiana na sarufi ya lugha ya Kimakonde. Ingawa utafiti huo haukulenga kuonesha vibainishi vioneshi, alitoa fasili ya vibainishi vioneshi. Kraal (keshatajwa) anafasili vibainishi vioneshi kuwa ni maneno ambayo yamejengeka katika sifa ya kuonesha kitu fulani ama cha karibu au mbali na eneo la mzungumzaji na msikilizaji. Kraal ametoa mifano kutoka katika lugha ya Kimakonde kama vile *ayu (*huyu), *aneyo (*huyo) na *ayula (*yule). Ukichunguza mifano ya vibainishi hivi vya Kimakonde, vinaonekana kuwa vina umbo maalum, vina dhima na vinaweza kuchanganuliwa kimofolojia.

Aidha, Khamis (2011) anafasili vibainishi vioneshi katika lugha ya Kiswahili kuwa ni neno lenye kufanya kazi ya kuonesha sehemu ya karibu au mbali. Kwa mfano:

3 (i) Mtaalamu **huyu** ni mwenzetu.
(ii) Kamba **hii** ni ndefu sana.
(iii) **Hao** wanafunzi wamelipa ada zao.

**Chanzo:** Khamis (2011)

[1] Neno kibainisho ni tafsiri ya neno la Kiingereza "articles."

Katika mfano wa 3, maneno yaliyokozwa wino ni vibainishi vioneshi katika sentensi hizo. Vibainishi hujitokeza baada au kabla ya nomino, kama mifano inavyojipambanua hapo juu.

Licha ya wataalamu hawa kujadili dhana ya vibainishi vioneshi katika lugha za Kibantu, hawajatofautiana na wataalamu waliofasili dhana ya vibainishi vioneshi katika lugha nyingine ulimwenguni kama vile lugha ya Kiingereza. Mathalani, Richards na Schmidt (2002) wanafasili vibainishi vioneshi kuwa ni neno ama kiwakilishi, kivumishi au kioneshi ambacho hutaja kitu fulani ama kikiwa karibu au mbali kutoka kwa wazungumzaji. Kwa mfano, katika lugha ya Kiingereza ni *this* (huyu) *that* (yule), *these* (hawa) na *those* (wale). Ukichunguza maumbo ya vibainishi vioneshi hivi katika lugha ya Kiingereza havina umbo linaloweza kuchanganuliwa kimofolojia kwa kuvunjwavunjwa zaidi. Jambo hili ni tofauti na maumbo ya vibainishi vioneshi vya Kiswahili ambayo yamedhihirika kwamba ni maalum na yanayochanganulika kwa mujibu wa makala hii.

Aidha, kuna baadhi ya wataalamu wamefasili kwa mtazamo tofauti dhana hii ya vibainishi vioneshi ukilinganisha na wataalam waliotangulia. Kwa mfano, Wesana-Chomi (2013) anafafanua kuwa, vibainishi vioneshi ni aina ya vivumishi vionyeshi katika lugha. Hii ina maana kwamba vibainishi vioneshi ni mojawapo ya vivumishi. Fasili ya Wesana-Chomi inatuelekeza kutuaminisha kwamba vibainishi vioneshi ni miongoni mwa aina ya vivumishi.

Kadhalika Thomson na Schleicher (2001) wanafasili dhana ya vioneshi wakihusisha na vibainishi vioneshi kwa kusema kwamba vibainishi vioneshi ni viwakilishi vioneshi au vivumishi vionyeshi katika sentensi. Kwa mfano, *wale, hivi* na *kule*. Wanaendelea kufafanua kwamba vibainishi ni vipashio ambavyo vikikaa katika sentensi hufanya kazi ya vivumishi vioneshi au viwakilishi vioneshi; yaani vikitokea katika nafasi ya nomino hufanya kazi ya kiwakilishi ilhali vikikaa baada ya nomino hufanya kazi ya kivumishi. Fasili ya Thomson na Schleicher imetofautiana kidogo na fasili ya Wesana-Chomi (*keshatajwa*) kwa kuongeza kipengele cha viwakilishi katika dhana ya vibainishi vioneshi katika lugha ya Kiswahili. Hali hii inatokana na kutoa fasili ya vibainishi vioneshi kutegemea nafasi ya vibainishi hivyo katika tungo.

Habwe na Karanja (2012) wanafafanua dhana ya vibainishi vioneshi kwa kusema kwamba katika Kiswahili vibainishi vioneshi vinapotokea kabla ya nomino hufanya kazi ya vibainisho. Maelezo ya Habwe na Karanja yanaonyesha kwamba maumbo ya vioneshi katika lugha ya Kiswahili ni sawa na vibainishi vioneshi. Ukichunguza fasili za wataalamu hawa, utabaini kuwa zimeegemea katika kigezo cha kisintaksia, ambacho huanisha neno kwa kuangalia nafasi yake katika tungo. Kama ilivyoelezwa awali, makala haya yanavichukulia vibainishi vioneshi kuwa ni kategoria ya neno inayojitegemea kama zilivyo aina nyingine za maneno. Hivyo basi, kwa mujibu wa makala hii, kibainishi kioneshi ni kategoria ya neno inayobainisha neno jingine hususan nomino na inaweza kuonesha mahali, msisitizo, kuhimiza na kuonesha umbali au ukaribu.

**Muundo wa Vibainishi Vioneshi**

Kwa mujibu wa TUKI (2013), muundo ni umbo la kitu kutokana na jinsi kilivyoundwa au kutengenezwa. Katika makala haya tumeitumia dhana ya muundo tukimaanisha mpangilio wa vipashio vinavyohusika kujenga vibainishi vioneshi vya Kiswahili. Vibainishi vioneshi, kama mojawapo ya kategoria za maneno, vina muundo wake ambao hutofautiana na aina nyingine za maneno kama vile nomino, vivumishi, vitenzi na vielezi. Hali kadhalika, kategoria hii ya vibainishi vioneshi hutofautiana kimuundo baina ya lugha moja na nyingine. Data ya vibainishi vioneshi vilivyotumika katika makala haya ni sehemu ya data iliyokusanywa mwaka 2018 kutoka katika vitabu teule kama ilivyofafanuliwa awali katika kipengele cha utangulizi. Lifuatalo ni jedwali linaloonesha vibainishi vioneshi katika muktadha wa kimatumizi.

**Jedwali 1: Vibainishi Vioneshi katika Muktadha wa Kimatumizi**

| Ngeli | Vibainishi Vioneshi vya Karibu na Mzungumzaji | Vibainishi Vioneshi vya Mbali na Mzungumzaji | Vibainishi Vioneshi vya Mbali na Mzungumzaji na Msikilizaji |
|---|---|---|---|
| 01 | Msichana ***huyu*** uk 1 | Kiumbe ***huyo*** uk 2 | ***Yule*** msichana uk 5 KM |
| 02 | Majirani ***hawa*** uk 155 | Vijana ***hao*** uk 11 | ***Wale*** wanawake uk 109 KM |
| 03 | Mchezo ***huu*** uk 1 | Mhimili ***huo*** uk uk 72 | ***Ule*** muujiza… uk 102 KM |
| 04 | Hali ***hii*** uk 12 | Sauti ***hiyo*** uk 117 | ***Ile*** nafsi yake uk 124 KK |
| 05 | Jambo ***hili*** uk 6 | ***Hilo*** nalijua uk 29 | Sanamu ***lile*** uk 185 KM |
| 06 | Maneno ***haya*** uk 13 | Ukaacha ***hayo*** uk 88 | …***yale*** mambo uk 36 KM |
| 07 | Kitabu ***hiki*** uk 164 | ..kwenye kiti ***hicho*** uk 120 | Naogopa ***kile*** uk 124 KK |
| 08 | Miezi mitatu ***hivi*** uk 4 | Basi ***hivyo*** ndivyo ilivyo uk 61 | Tulifanya ***vile*** uk 9 KM |
| 09 | Nchi ***hii*** uk 1 | Tutolee hadithi ***hiyo*** uk 6 | ***Ile*** sauti uk 117 KK |
| 10 | Siku ***hizi*** uk 6 | ***Haya*** lete hizo shahada uk 12 | Siku ***zile*** uk 86 KK |
| 11 | Mchanga ***huu*** uk 9 | Muda wote ***huo***? uk 83 | ***Ule ule*** uk 111 KK |
| 12 | Siku ***hizi*** uk 104 | Kelele ***hizo*** uk 121 | ***Zile*** pale uk 107 KK |
| 13 | Wakati ***huu*** uk 106 | ***Huo*** mpunga.. uk 19 | Wakati ***ule*** uk 172 KM |
| 14 | Mafumbo ***haya*** uk 122 | Na ***hayo***…uk 22 | Mambo ***yale yale*** uk 128 KM |
| 15 | Njooni ***huku*** uk 179 | …na mtu ***huko*** juu uk 91 | Kokote ***kule*** uk 90 KK |
| 16 | Limetuleta ***hapa*** uk 172 | Macho yako ***hapo*** | ***Pale*** shuleni uk 8 KM |
| 17 | Rudini ***huku*** uk 188 | Umenipeleka ***huko*** uk 120 | ***Kule*** mtoni uk 45 KM |
| 18 | ***Humu humu*** mjini | Utatibiwa ***humo*** ndani Uk 124 | ***Mule*** ndani uk 61 KK |
| | **Chanzo**:K*ichwamaji* (KM) (Kezilabi, 1974) | **Chanzo**: *Kivuli Kinaishi* (KK) (Mohamed, 1990) | |

**Chanzo:** Data kutoka maktabani, 2018

Katika lugha ya Kiswahili, muundo wa vibainishi vioneshi hutofautiana kutoka aina moja ya kibanishi kioneshi hadi nyingine. Data zilizokusanywa ziligawanywa katika makundi matatu ya vibainishi vioneshi katika lugha ya Kiswahili ambayo hutofautiana kimuundo. Makundi hayo ni vibainishi vioneshi vya mbali na mzungumzaji; vibainishi hivi hujishughulisha na kutambulisha nomino au kategoria nyingine ya maneno ambayo iko mbali kidogo na mzungumzaji lakini kategoria hiyo ikiwa iko karibu na msikilizaji. Vibainishi vioneshi vya karibu na mzungumzaji hutumika kubainisha nomino ambayo iko karibu na mzungumzaji ilhali vibainishi vioneshi vya mbali na mzungumzaji na msikilizaji huonesha umbali uliopo baina ya mzungumzaji na msikilizaji na mtu au kitu kinachotajwa. Iwapo kitakuwa kitu basi kinaweza kuwa kitu kilicho dhahiri au dhahania katika mazingira ya mzungumzaji na msikilizaji.

Baada ya kuchunguza data zilizokusanywa katika makala hii, imebainika kwamba muundo wa vibainishi vioneshi vya Kiswahili unafuata utaratibu maalum na huukiliwa na mfumo wa ngeli zinazohusika. Tukianza na muundo wa vibainishi vioneshi vya karibu na mzungumzaji, imebainika kuwa vibainishi hivi hutawaliwa na mzizi {h-} ukifuatiwa na irabu mwangwi iliyonakiliwa kutoka katika kiambishi ngeli cha kibainishi husika na mwisho hukaa kiambishi ngeli cha ngeli hiyo. Pili, vibainishi vioneshi vya mbali na mzungumzaji navyo hutawaliwa na mzizi {h-} ambao hufuatiwa na irabu mwangwi. Mwisho, huambikwa kiambishi rejeshi -o ambacho hujitokeza mwishoni mwa kila kibainishi. Tatu, vibainishi vioneshi vya mbali na mzungumzaji na msikilizaji huundwa na mzizi {-le} ambao hujitokeza mwishoni mwa kibainishi kinachohusika ukitanguliwa na viambishi ngeli vya nomino husika. Matokeo haya yanashadadia tafiti tangulizi zenye mrengo unaounga mkono miundo hii na kubatilisha tafiti zilizoshadidia muundo kama uliopendekezwa na Wesana-Chomi, rejea utafiti wa Champunga (2018).

Makala haya yamebaini kuwa katika lugha ya Kiswahili, muundo wa vibainishi vioneshi hutofautiana kutoka aina moja ya vibainishi vioneshi hadi nyingine. Hii ina maana kwamba kila aina ya vibainishi hivyo ina muundo wake. Miundo hii imeoneshwa kwa muhtasari katika jedwali namba 2 kwa kuteua kibainishi kimoja kutoka katika kila aina vya vibainishi vioneshi vya Kiswahili.

**Jedwali 2: Muhtasari wa Muundo wa Vibainishi Vioneshi vya Kiswahili**

| **Aina za Vibainishi** | **Muundo wa Vibainishi Vioneshi** | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kibainishi Kioneshi** | **Mz** | **Irabu Akisi** | **KNg** | **Mz** |
| Cha Mbali na Mzungumzaji | h- | -u- | -yo | |
| Cha Karibu na Mzungumzaji | h- | -a- | -wa | |
| Cha Mbali na Mzungumzaji na Msikilizaji | | | yu- | -le |

**Chanzo**: Data ya utafiti (2018)

Data katika jedwali namba 2 inaonesha muhtasari wa muundo wa vibainishi vioneshi vya Kiswahili. Pia, uchunguzi wa data umeonesha kwamba, katika lugha ya Kiswahili, vibainishi vioneshi hufungamana na mazingira mbalimbali ya utokeaji wake. Kauli hii ina maana kwamba kibanishi kinaweza kutokea kabla au baada ya nomino kutegemea lengo la mzungumzaji katika muktadha wa mazungumzo.

**Dhima za Vibainishi Vioneshi vya Lugha ya Kiswahili**

Utafiti huu, umebaini kuwa ni vigumu kupata dhima za vibainishi vioneshi bila kuhusisha mkabala wa kisintaksia. Kwa hiyo, mara nyingi dhima huchanuza zaidi pale vibainishi hivyo vikiwa katika tungo, katika lugha ya mazungumzo au maandishi ambapo wazungumzaji huwa huru kutumia aina yoyote ya vibainishi vioneshi wanavyovijua ili kufanikisha dhamiri ya mawasiliano.

Kwa maelezo hayo, tunachotaka kusema ni kwamba ingawa utafiti huu unatumia mkabala wa kimofolojia, lakini katika sehemu hii tumebainisha na kujadili vipashio vya kisarufi kwa kujikita katika mofolojia na sintaksia. Kwa hiyo, tumeichukulia mofolojia kama mchakato na sintaksia kama mofolojia tendeshi kwani wakati mwingine katika isimu ni vigumu kutenganisha maumbo ya kimofolojia bila kutumia mifano ya miundo ya kisintaksia hasa katika kiwango cha kuelezea dhima. Hivyo, kwa kutumia mhimili wa kuhifadhi muundo, ambao unasisitiza kuunda maneno yenye maana katika lugha, tuliweza kubainisha na kujadili dhima mbalimbali za vibainishi vioneshi.

**Dhima ya Kuonesha Mahali**

Vibainishi vioneshi hutumika kuonesha mahali. Dhima hii imeelezwa na wataalamu mbalimbali katika sarufi ya Kiswahili kama vile Kapinga (1983) na Mohammed (2001). Wataalamu hao wanafafanua kuwa vibainishi vioneshi hurejelea umahali bila kurejelea umbali na ukaribu.

Dhima ya kuonesha mahali ni miongoni mwa dhima ambazo zimejitokeza katika utafiti huu. Dhima hii huonyesha umahali kwa namna tatu tofauti. Kwanza, huonesha mahali mahsusi. Pili, hudokeza mahali pa jumla na tatu kudokeza mahali ndani ya kitu fulani. Namna hizi tatu, zinafafanuliwa katika dhima hii ya umahali.

Dhima ya umahali hujibainisha katika vibainishi vioneshi vinavyopatikana katika makundi matatu kutegemea viambishi ngeli vya upatanishi wa kisarufi ambavyo ni Pa (16), Ku (17) na Mu (18). Ngeli hizi huitwa ngeli za "mahali" ambazo hujitokeza karibu katika lugha zote za Kibantu (Maho, 1999). Kiambishi **pa** huonesha mahali mahsusi, kiambishi **ku** huonesha mahali pa jumla na kiambishi **mu** huonesha mahali ndani ya kitu. Viambishi hivi vinaweza kujitokeza mwanzo au mwishoni mwa kibainishi kutegemea aina ya vibainishi vioneshi vilivyotumika kubainisha mahali hapo. Data inayofuata inathibitisha vibainishi vioneshi vyenye dhima ya mahali mahsusi katika lugha ya Kiswahili kama ambavyo tumeikusanya katika matini tulizozichunguza:

4 (a) Yanayotokea *hapa* nyumbani (uk. 64)
(b) Sisi *hapa* (uk. 128)
(c) Yamesimama *pale* (uk. 133)

**Chanzo**: *Kichwamaji* (Kezilahabi, 1974)

5 (a) Utulivu wote wa *hapa* (uk. 12)

(b) Mwenyewe yupo *hapa* (uk. 60)

(c) Linazidi *hapo* (uk. 90)

**Chanzo:** *Kichwamaji* (Kezilahabi, 1974)

Data katika mfano namba (4) na (5) zinaonesha vibainishi vioneshi vya umahali *hapa*, *pale* na *hapo*. Vibainishi hivi vina dhima ya kuonesha mahali hususani mahali mahususi. Mara nyingi, vibainishi hivi huwakilishwa na kiambishi **pa**, umahali ukihusishwa na ukaribu wa mzungumzaji na msikilizaji, lakini hujitokeza kama **-po** ukiwa mahali ni mbali na mzungumzaji.

Data inayofuata ni mifano ya vibainishi vioneshi vyenye kuonesha dhima ya mahali pa jumla.

6 (a) Tulale *huko* ndani (uk. 3)

(b) *Huku* Ukerewe (uk. 104)

(c) Nimngoje *kule* mbele…. (uk. 88)

**Chanzo:** *Kichwamaji* (Kezilahabi, 1974)

7 (a) Anakwenda *huku* na kurudi *huku* (uk. 72)

(b) …niwaite niungane nao *huko* waliko (uk. 75)

(c) *Kule* kuliko na uzito… (uk. 117)

**Chanzo:** *Kivuli Kinaishi* (Mohamed, 1990)

Katika mifano namba 6 na 7 tunaona vibainishi vioneshi *huku*, *huko* na *kule* vyenye dhima ya kuonesha mahali pa jumla. Vibainishi hivi hujidhihirisha na viambishi **ku/ko** ambayo huweza kujitokeza mwishoni au mwanzoni mwa kibainishi kioneshi kutegemea aina ya kibainishi kioneshi kinachotumika.

Data inayofuata katika namba 8 na 9 inaonesha vibainishi vioneshi vyenye dhima ya mahali ndani ya kitu fulani.

8 (a) …kuishi *humu* mjini (uk. 171)

(b) *Humo* ndani, *humo humo* garini (uk. 183)

(c) *Mule* ndani (uk. 183)

**Chanzo:** *Kichwamaji* (Kezilahabi, 1974)

9 (a) Niliweka *humu* (uk. 18)

(b) *Humo* kibuyuni (uk. 46)

(c) Yuko *mule* (uk. 46)

**Chanzo:** *Kivuli Kinaishi* (Mohamed, 1990)

Katika data yetu hapo juu, tunaona vibainishi vioneshi *humu*, *humo* na *mule*. Hivi ni vibainishi vioneshi vyenye dhima ya kuonesha mahali ndani ya kitu fulani, aghalabu kitu hicho huwa ni nomino za mahali au viwakilishi. Aina hii ya vibainishi hutawaliwa na kiambishi **mu** ambacho hujitokeza mwanzoni au mwishoni mwa kibainishi hicho. Hujitokeza ikiwa umahali huo umebainishwa kwa kuzingatia umbali wa mzungumzaji na msikilizaji. Kiambishi **mu** hubadilika kuwa na kuwa kiambishi **mo** ikiwa mahali kunakorejelewa ni mbali na mzungumzaji.

**Dhima ya Kuonesha Masafa**

Dhima ya kuonesha umbali au ukaribu wa kitu ni miongoni mwa dhima ambazo zimebebwa na vibainishi vioneshi vya Kiswahili. Ukaribu hutegemea nafasi ya mzungumzaji na msikilizaji na kitajwa. Iwapo mzungumzaji yuko karibu na kitajwa, dhima ya kibainishi hiki huwa ni kuonesha ukaribu wa mzungumzaji na kinachozungumziwa (kitajwa). Mfano wa maumbo ya vibainishi vioneshi ambayo huchanuza dhima ya vibainishi vya karibu na mzungumzaji ni *huyu, hiki, hawa* na *hapa*. Dhima ya umbali hujitokeza iwapo kitajwa kinakuwa mbali na mzungumzaji pekee au mbali na wote wawili (mzungumzaji na msikilizaji). Mifano namba 10 na 11 inaonesha namna dhana hii inavyojidhihirisha katika vibainishi vya Kiswahili.

10 (a) mchezo *huu* (uk. 1)
(b) Shitaka *hili* (uk. 81)
(c) *huyu hapa* (uk. 119)

**Chanzo:** *Kichwamaji* (Kezilahabi, 1974)

11 (a) mpunga wenyewe ni *huu* (uk. 18)
(b) niliweka *humu* (uk. 19)
(c) rangi *hii* (uk. 101)
(d) umewapa nini *hawa*? (uk. 109)

**Chanzo:** *Kivuli Kinaishi* (Mohamed, 1990)

Data hii inaonesha ujitokezaji wa dhima ya ukaribu wa mzungumzaji na kitu kinachorejelewa katika mazingira halisi. Maumbo yaliyo katika hati mlalo ndiyo vibainishi vioneshi vya karibu na mzungumzaji. Hii ndiyo dhima ambayo imezungumziwa na wataalamu wengi wa sarufi ya Kiswahili katika kuonesha dhima ya vibainishi katika lugha ya Kiswahili (taz. k.m. Polomé, 1967; Massamba, 2004; Thompson na Schleicher, 2001; Wesana-Chomi, 2013).

Licha ya kuwapo kwa dhima ya kuonesha ukaribu, makala haya yamebaini kuwapo kwa dhima ya umbali ambayo inabebwa na vibainishi vioneshi vya Kiswahili. Umbali huu hujitokeza katika miktadha miwili. Umbali uliopo baina ya mzungumzaji na kitajwa na umbali uliopo baina mzungumzaji na msikilizaji. Mifano katika namba 12 na 13 inaonesha dhima ya umbali na mzungumzaji na katika namba 14 na 15 ni mifano ya dhima ya vibainishi vioneshi vya umbali na mzungumzaji na msikilizaji:

12 (a) wasichana *hao* (uk. 6)
(b) *hapo hapo* (uk. 45)
(c) swali kama *hilo* (uk. 64)
(d) *humo* mlimani (uk. 133)

13 (a) *yule* mzee (uk. 2)
(b) *kule* mtoni (uk. 45)
(c) *ile ile* (uk. 96)
(d) sanamu *lile* (uk. 185)

**Chanzo:** *Kichwamaji* (Kezilahabi, 1974)

14 (a) *huo* mpunga
(b) *huko* Giningi (uk. 82)
(c) ndoto *hiyo* (uk. 110)

15 (a) hasa *wale* vijana (uk. 10)
(b) mleteni *yule* (uk. 65)
(c) unatambua *pale* (uk. 86)

**Chanzo:** *Kivuli Kinaishi* (Mohamed, 1990)

Katika data (12-15) maumbo ya maneno yaliyopo katika hatimlalo ni vibainishi vioneshi vya Kiswahili vinavyobainisha dhima za umbali. Yale yaliyo katika data namba (12) na (14) yanaonesha dhima za umbali na mzungumzaji; ikiwa na maana kwamba kitajwa kipo mbali na mazingira aliyopo mzungumzaji lakini kipo karibu na msikilizaji. Kwa upande mwingine, maumbo mlalo yaliyo katika data namba (13) na (15) yanaonesha dhima za umbali wa mzungumzaji na msikilizaji, ikiwa na maana kwamba kinachorejelewa kinakuwa mbali na wote wawili.

**Dhima ya Kuonesha Msisitizo**

Kusisitiza ni kutia mkazo katika maelezo, habari au jambo lolote ili kuonesha jinsi jambo lenyewe lilivyo muhimu (TUKI, 2013). Kuonesha msisitizo ni miongoni mwa dhima za vibainishi vioneshi katika lugha ya Kiswahili kulingana na makala hii. Data katika mfano namba 16 na 17 inaonesha namna dhima hii inavyojidhihirisha.

16 (a) *huyo huyo* (uk. 14)

(b) wakati *huo huo* niliona moshi…. (uk. 25)

(c) "… Huyu mwendawazimu," alijibu. "Manase?" "*Huyo huyo*". (uk. 25)

*(d)* "…wanaishi kijijini *humu humu (*uk. 30)

(e) Tumekutana naye nijani anatoka *huko huko* (uk. 35)

**Chanzo:** *Kichwamaji* (Kezilahabi, 1974)

17 (a) Yaishe *hapa hapa* (uk. 18)

(b) Hatukuja *hivi hivi* sisi (uk. 28)

(c) Namna *ile ile* (uk. 65)

(d) "...Wapo *palepale* (uk. 77)

(e) "… ni *yale yale* (uk. 98)

**Chanzo:** *Kivuli Kinaishi* (Mohamed, 1990)

Data katika 16 na 17 inaonesha kuwa vibainishi vioneshi katika Kiswahili pia vina dhima ya kuonesha msisitizo. Dhima hii hujichanuza pale vibainishi vya Kiswahili vinaporadidiwa. Dhima hii pia inapatikana katika lugha nyingine za Kibantu, mathalani lugha ya Kibena (Morrison, 2011), ingawa zipo tofauti ndogondogo. Kwa mfano, katika lugha ya Kibena, msisitizo huoneshwa kwa umbo moja tu bila uradidi ilhali katika lugha ya Kiswahili vibainishi vinavyotekeleza dhima hiyo ni lazima viradidiwe.

**Dhima ya Urejeshi**

Baadhi ya vibainishi vioneshi vya Kiswahili vilivyochunguzwa vimedhihirika kuwa na dhima ya urejeshi. Kulingana na data zilizokusanywa, dhima hii hujidhihirisha kwenye mazingira ya tungo zinazohusiana na wakati uliopita kama tunavyoweza kuona katika data za mifano ya 18 na 19.

18 (a) kulikuwa bado watu wawili, *yule* mzee na msichana mmoja (uk. 2)

(b) mkononi mwake alikuwa ameshika bado *kile* kikaratasi nilichompelekea (uk. 110)

(c) nilikumbuka siku *ile* nilipokwenda kumtembelea kamata (uk. 130)

(d) alijaza *lile* bakuli la pili akalipeleka jikoni (uk. 171)

(e) uliyahifadhi maisha yangu wakati *ule*… (uk. 172)

**Chanzo**: *Kichwamaji* (Kezilahabi, 1974)

19 (a) …anaonekana ana hadhi zaidi kuliko *yule* wa mwanzo (uk. 17)

(b) *Ile* mbegu mliyoipanda… (uk. 99)

(c) Au ni *kile* kivuli nilichokuwa nikihisi na kukiona… (uk. 117)

(d) … na *ile* sauti niliyoisikia kwa mtekenyo wa hewa (uk. 117)

(e) … leo ndiyo *ile* siku yetu na yako (uk. 127)

**Chanzo**: *Kivuli Kinaishi* (Mohamed, 1990)

Katika mifano ya data namba 18-19 tunaona maumbo tofauti ya vibainishi vioneshi. Maumbo hayo ni *ile, yule, kile* na kadhalika ambayo yanapatikana katika kundi la vibainishi vioneshi vya mbali na mzungumzaji na msikilizaji. Licha ya kuonesha umbali makala haya yamebaini pia kwamba wakati mwingine vibainishi vioneshi hurejelea jambo lililotajwa kabla katika mazungumzo au masimulizi. Tuchunguze mifano ifuatayo:

20 (a) Jioni *hiyo*
(b) Mchezo *huo*
(c) Wakati *huo*
(d) Asubuhi *hiyo*
(e) Jambo *hilo*

**Chanzo:** *Kichwamaji* (Kezilahabi, 1974)

21 (a) Ugumu wa neno *hilo* (uk. 7)
(b) Elimu yote *hiyo* mnayopewa (uk. 23)
(c) mhimili *huo* (uk. 72)
(d) zaidi ya *hapo* (uk. 111)

**Chanzo:** *Kivuli Kinaishi* (Mohamed, 1990)

Data katika namba (20) na (21) inaonesha kuwa vibainishi vioneshi vya Kiswahili vya karibu na msikilizaji, vya mbali na mzungumzaji vina tabia ya kuonesha kitajwa kilichokwishatajwa awali. Matokeo haya si mapya kwani tafiti tangulizi pia zinataja dhima hii. Palome (1967) na Ashton (1944) kwa mfano, wanafafanua kuwa kwa kawaida vibainishi vioneshi vinavyoanza na mzizi {h-} na kuishia na irabu {-o} huonesha kitu kilichotajwa awali. Kwa hiyo makala haya yanathibitisha matokeo ya tafiti zilizotangulia, jambo ambalo linazipa tafiti hizo uthabiti zaidi.

**Dhima ya Kukubali au Kuitikia**

Dhima ya kukubali au kukiri jambo ni miongoni mwa dhima za vibainishi vioneshi vya karibu na mzungumzaji katika lugha ya Kiswahili iliyobainishwa na makala hii. Aghalabu, dhima hii huonesha hali ya kukubali jambo fulani. Baadhi ya vibainishi vioneshi vya karibu na mzungumzaji vilivyochunguzwa katika makala haya vimedhihirika kuwa na dhima madhukura. Dhima hii hujipambanua hasa katika ngeli ya 6 na 14. Data katika mifano namba 22 na 23 inaonesha dhima hiyo.

22 (a) *Haya* kwaheri (uk. 6)
(b) Halafu sauti ndogo ilitoka. "*Haya*". (uk. 53)
(c) *Haya* nitajaribu (uk. 62)
(d) *Haya* chukua! (uk. 71)

**Chanzo:** *Kichwamaji* (Kezilahabi, 1974)

23 (a) Bora sema sauti ya nini tena? *Haya* sa… sau… sauti ya nini tena?
(b) Mking'ang'ania *haya*! Nitawasimulieni (uk. 7)
(c) *Haya* subiri (uk. 7)

**Chanzo:** *Kivuli Kinaishi* (Mohamed, 1990)

Katika data za mfano wa (22-23) data inaonesha, dhima ya vibainishi vioneshi ya kukubali jambo inadhihirika. Umbo linalochagiza dhima hii hujitokeza mwanzoni au mwishoni mwa tungo. Pia, huweza kufuatiwa na aina yoyote ya maneno kama vile; nomino, kitenzi au kihusishi. Kama inavyodhihirika katika data namba 29 na 30 umbo hili (***haya***) licha ya kufanya kazi ya kuonesha mwitikio wa jambo au kukubali jambo fulani kama ilivyojadiliwa katika makala hii, huweza kuchanuza dhima nyingine ya kuhimiza jambo. Dhima hii imefafanuliwa katika sehemu inayofuata.

**Dhima ya Kuhimiza**

Kuhimiza ni mojawawapo ya dhima za vibainishi vioneshi vya Kiswahili. Dhima hii huhusisha vitendo vya kumtia moyo mtu anayetenda jambo ili aweze kulitenda au alifanye kwa kuharakisha. Baadhi ya vibainishi vioneshi, hasa vya karibu na mzungumzaji hufanya hiyo kazi kama inavyodhihirika katika data namba 24 na 25.

24 (a) *Haya* kaeni! (uk. 9)

(b) *Haya* nenda nyumbani (uk. 134)

**Chanzo:** *Kichwamaji* (Kezilahabi, 1974)

25 (a) *Haya*…. Haya nyanyueni gilasi (uk. 36)

(b) *Haya* sasa nyanyueni vifua vyenu taratibu (uk. 37)

(c) *Haya* sasa tikiseni vichwa vyenu taratibu (uk.38)

(d) *Haya* sasa fuateni mdundo wa ngoma (uk. 38)

(e) *Haya* damkeni, taratibu…

**Chanzo:** *Kivuli Kinaishi* (Mohamed, 1990)

Data katika namba mifano namba 24-25 zinaonesha kuwa vibainishi vioneshi vina dhima ya kuhimiza jambo. Vibainishi vioneshi vya karibu na mzungumzaji vyenye dhima ya kuhimiza jambo vimebainishwa kutokea katika ngeli 6 na 14. Vibainishi vioneshi hivi vikikaa mwanzoni mwa tungo hufanya kazi ya kuonesha dhima ya kuhimiza jambo fulani.

**Dhima ya Ukadiriaji**

Ukadiriaji ni ukisiaji wa kiasi kinachofaa bila kuzidi wala kupungua (TUKI, 2013). Hivyo, baadhi ya vibainishi vioneshi vilivyochunguzwa katika lugha ya Kiswahili vinadokeza dhima ya ukadiriaji kama data namba 26 na 27 zinavyodhihirisha.

26 (a) Miezi mitatu *hivi* (uk. 4)

(b) Thelathini *hivi* (uk. 4)

(c) Kama kumi *hivi* (uk. 8)

(d) Dakika kumi *hivi* (uk. 100)

(e) Matatu hivi (uk.145)

**Chanzo:** *Kichwamaji* (Kezilahabi, 1974)

27 (a) Utakwisha punde *hivi*… (uk. 117)

**Chanzo**: *Kivuli Kinaishi* (Mohamed, 1990)

Data katika namba (26) na (27) inadhihirisha wazi kuwa baadhi ya vibainishi vioneshi katika lugha ya Kiswahili huwa na dhima ya ukadiriaji. Makala haya yamebaini kwamba dhima hii hujitokeza katika vibainishi vya karibu na mzungumzaji, hususan katika ngeli ya 8 (***hivi***) kinapotokea baada ya nomino.

**Dhima ya Uunganishaji**

Kiunganishi ni neno linalounganisha maneno, vikundi vya maneno au sentensi (TUKI, 2013). Dhima kuu ya kiunganishi ni kuweka pamoja vipashio viwili au zaidi vyenye hadhi sawa kisarufi ili kuunda kipashio kimoja. Katika lugha ya Kiswahili, viunganishi vinaweza kuwa vya jina kwa jina, kitenzi kwa kitenzi, kirai kwa kirai, kishazi kwa kishazi pamoja na sentensi kwa sentensi. Kulingana na data ya makala hii, baadhi ya vibainishi vioneshi vya Kiswahili vinadokeza dhima ya kuunganisha, hususan vile vinavyopatikana katika ngeli ya 15 na 17 kama inavyoonekana katika data namba 28 na 29.

28 (a) Niache, alisema *huku* akicheka (uk. 32)

(b) Aliendelea *huku* akiweka mkono wake…. (uk. 82)

(c) "…karibu na moto *huku* miguu yake…" (uk. 144)

(d) Alisema *huku* akimpiga begani (uk. 170)

**Chanzo:** *Kichwamaji* (Kezilahabi, 1974)

29 (a) Anasema *huku* akienda (uk. 62)

(b) Anakwenda *huku* akirudi huku (uk. 69)

(c) Zinafifia *huku* zikisema kwa mwangwi… (uk. 89)

(d) Kuingiliana *huku* wakifukuzana (uk. 104)

(e) Anapiga kelele na kulia *huku* akijibanza pembeni (uk. 128)

**Chanzo:** *Kivuli Kinaishi* (Mohamed, 1990)

Data katika namba (28) na (29) zinaonesha kuwa baadhi ya vibainishi vioneshi vya Kiswahili vinadokeza dhima ya kuunganisha vipashio mbalimbali. Vibainishi vioneshi hivi, licha ya kuwa na dhima ya kudokeza nomino za ngeli ya 15 na kudokeza mahali, hufanya kazi ya kuunganisha kama inavyoonekana katika data namba (28) na (29). Umbo linalojitokeza ni *huku* ambalo hujipambanua katika vibainishi vioneshi vya karibu na mzungumzaji.

**Hitimisho**

Katika kuhihimisha lengo la makala haya ambalo lilikuwa ni dhima za vibainishi vioneshi, imebainika kwamba zipo dhima mbalimbali za vibainishi vioneshi katika lugha ya Kiswahili. Miongoni mwa dhima hizo ni kuhimiza, kusisitiza, kurejesha, kukubali au kuitikia, kuunganisha na kukadiria. Aidha, vibainishi vioneshi hudokeza pia dhima ya kuonesha umbali na ukaribu wa kitu na kuonesha umahali. Pia, imebainika kwamba dhima za vibainishi vioneshi hutokana na muktadha wa matumizi kulingana na hali ya mazungumzaji. Kwa hiyo, dhima za vibainishi vioneshi katika lugha ya Kiswahili hufungamana na muktadha wa kimazungumzo na kimasimulizi. Jambo jingine lililodhihirishwa na makala haya ni kwamba hakuna mipaka ya moja kwa moja kati ya dhima anuwai za vibainishi vioneshi zinazochanuzwa katika lugha ya Kiswahili kwa sababu umbo la kibainishi kioneshi kimoja katika sentensi linaweza kuchanuza dhima zaidi ya moja. Tukiangalia tafiti zilizotangulia, matokeo ya utafiti huu, yanaunga mkono dhima ya kuonesha umbali au ukaribu wa kitu kama ilivyowakilishwa na wataalamu mbalimbali kama akina Thompson na Schleicher (2001). Tofauti na matokeo ya tafiti za awali, makala haya yanaeleza kuwapo kwa dhima mbalimbali za vibainishi katika lugha ya Kiswahili na kubatilisha mtazamo wa kuwapo kwa dhima moja ya vibainishi vioneshi uliowasilishwa awali na wataalamu kama Thompson na Schleicher (2001) na Wesana-Chomi (2013).

## Marejeleo


Ashton, E. O. (1944) *Swahili Grammar Including Intonation*. London: Longman.

Buberwa, A. (2014). Ruwaza za Kimofolojia za Majina ya Mahali ya Kihaya: Mtazamo wa Mofolojia Leksika. Katika *Kiswahili* Juz. 77. uk. 41-61.

Buberwa, A. (2016). "Mofolojia ya Majina ya Mahali ya Kiswahili na Kihaya katika Jamii ya Wahaya: Uzingativu wa Masuala ya Kiisimu Jamii." Tasnifu ya Uzamivu (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Champunga, S. I. (2018). Muundo na Dhima za Vibainishi Vioneshi katika Kiswahili Sanifu, Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Chomsky, N. (1965). *Aspect of the Theory of Syntax*. Cambridge: Massachusetts MIT Press.

Habwe, J na Karanja, P. (2012). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers..

Kapinga, M. C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Katamba, F. and Stonham, J. (2006). Morphology. Palgrave: Macmillan Education.

Kezilabahi, E. (1974). *Kichwamaji*. Dar es Salaam: East African Publishing House.

Khamis, A. A. (2011). Uchambuzi wa Kiswahili Fasaha. Chikwani: Chuo Kikuu cha Elimu Zanzibar.

Kihore, Y.M., Massamba, D.P.B. na Msanjira, Y.P. (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili*. Dar es salaam: TUKI.

Kiparsky, P. (1982). "Leksical Morphology and Phonology." Katika Yang, I.S (mh.) *Linguistics in the Morning Calm*. Seoul: Hanshin.

Kraal, P. (2005). A Grammar of Makonde in Chinnima dialect. Tasnifu ya Uzamivu (haijachapishwa). Leiden University.

Maho, J. F. (1999). *A Comparative Study of Bantu Noun Classes*. Acta Universitatis: Gothoburgensis.

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia, na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers (Kenya) Ltd.

Mohamed, M. A. (2001). *Modern Swahili Grammar*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mohamed, S. A. (1990). *Kivuli Kinaishi*. Nairobi: Oxford University Press.

Morrison, M. E. (2011). A Reference Grammar of Bena. Tasnifu ya Uzamivu (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Rice.

Mwamzandi, M. (2018). "A Corpus Study of the Swahili Demonstration Position": Selected paper from the 4th Annual Conference on African Linguistics. Katika *African. Linguistics.* uk 413-429.

Philipo, Z. (2015). "Tofauti baina ya Vivumishi na Vibainishi katika Lugha ya Kiswahili." Katika *Kioo cha Lugha*, Juz.13 uk. 125-143.

Polomé, E.C. (1967). *Swahili Language Handbook*. Washngton D.C: The Center for Applied Linguistics.

Richards, J. C. na Schmidt, R. (2002). *Longman Dictionary of Language Teaching and Applied Linguistics*: *Toleo la tatu*, London: Pearson Education Limited.

Strom, E. B. (2015) The Word Order in Swahili Adnominal Constructions with Locative Demonstratives. Katika *Nordic Journal of African Studies*. Juz 24 (2): uk 118-145.

Thompson, K. D. na Schleicher, A. F. (2001). *Swahili Leaners Reference Grammar*. Madison: NLRC Press.

Timoth, W. (1987). Discourse Distances and Swahili Demonstratives. Katika *Studies in African Linguistics*. Juz 18 (1). uk 81-95.

TUKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Toleo la Tatu. Nairobi: Oxford University Press.

Van de Velde, M. (2005). "The Order of Noun Demonstrative in Bantu." Katika *Studies in African Comperative Linguistics with Special Focus on Bantu and Mande.* (wah.) uk. 425-441.

Wesana- Chomi, E. (2013). *Kozi Tangulizi katika Sarufi Miundo ya Kiswahili.* Sebha: Chuo Kikuu cha Sebha.